3- الْوقْفُ الحَسَنْ Al-Waqf Al-Hasan - Kisimamo Kizuri (cha Kukubalika)

Ni kusimama katika yenye kutimiza maana yake, na yanafungamana na yanayofuatia kimaana na kilugha.

Hukmu Yake:

Inaruhusiwa kusimama katika kisimamo kama hichi, lakini haipendezi kuanzia na yanayofuatia; bali inapendekezwa na ni vizuri kurudia kusoma neno lililosimamiwa au kurudia neno au maneno ya nyuma yake ili ifungamane maana. Ama itakapokuwa kisimamo chenyewe ni mwisho wa Aayah basi wakati huo itapendeza kuanza na yanayofuatia bila ya kurudia neno au maneno.

Mifano ya الْوقْفُ الحَسَنْ **Al-Waqf Al-Hasan - Kisimamo Kizuri**

- Mfano wa kwanza mwishoni mwa Aayah:

  Kusimama katika kila Aayah kwenye Suwratul-Faatihah kama alivyokuwa akisoma Mtume (صلى الله عليه وسلم) ingawa kila Aayah inafungamana kimaana na kilugha na yanayofuatiana.

  ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ۝٢ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۝٣ مَٰلِكِ يَوْمِ ٱلدِّينِ ۝٤

  ((*Alhamduli-LLaah* [Sifa njema zote ni za Allaah] Mola wa walimwengu)) ((*Ar-Rahmaanir-Rahiym* [Mwingi wa Rehma - Mwenye kurehemu])) ((*Maalik* (Mfalme) wa siku ya malipo))

- Mfano wa pili mwishoni mwa Aayah:

  Kusimama kwenye mwisho wa Aayah inaleta maana sahihi kabisa lakini inafungamana na kinachofuatia mfungamano wenye nguvu wa kilugha na kimaana:

﴿ وَإِنَّكُمۡ لَتَمُرُّونَ عَلَيۡهِم مُّصۡبِحِينَ ١٣٧ وَبِٱلَّيۡلِۗ أَفَلَا تَعۡقِلُونَ ١٣٨ ﴾

((Nanyi bila shaka mnawapitia asubuhi)) ((Na usiku [pia mnawapitia] Je, basi hamtii akilini?))[1].

Bonyeza usikilize

Kwa maana: "Mnawapitia asubuhi na usiku pia mnawapitia"

- Mfano wa tatu mwishoni mwa Aayah:

﴿ فَوَيۡلٞ لِّلۡمُصَلِّينَ ٤ ﴿ ٱلَّذِينَ هُمۡ عَن صَلَاتِهِمۡ سَاهُونَ ٥ ﴾

((Basi ole kwa wanaoswali)) ((Ambao wanapuuza Swalah zao))[2]

Wanavyuoni wamekhitilafiana kuhusu kauli hiyo ya Allaah (سبحانه وتعالى)[3] kwa vile kuna waliokiona kuwa ni الْوَقْفُ الْقَبِيح Al-Waqf Al-Qabiyh (Kisimamo kinachochukiza au kibaya). Khitilafu hizo ni zifuatazo: (i) Haipasi kusimama ila kwa dharura na inawajibika kuunganisha na yanayofuatia. (ii) Inapasa kusimama kwa vile ni Sunnah iliyothibiti, lakini haipasi kuanza kwa Aayah inayofuatia bali linalotakiwa ni kuunganisha ili ilete maana iliyokusudiwa. (iii) Inapasa kusimamia kwa vile ni Sunnah iliyothibiti, na unaweza kuanza yanayofuatia lakini si kukata kisomo kabisa; yaani haipasi mtu kusimama hapo

---

[1] Asw-Swaaffaat (37: 137-138). Kusimama sehemu kama hizi kuna kauli mbili:

i- Inaruhusiwa kusimama na kisha kuanza na kinachofuatia bila ya kuwa na haja ya kurejea kusoma kilichokuwa kabla yake, kwa kuwa kisimamo kimetokea kwenye mwisho wa Aayah, na kusimama mwisho wa Aayah ni Sunnah iliyothibiti.

ii- Haipendezi kuanza (kusoma Qur-aan) na kinachofuatia bali itapendeza kukiwasilisha na kilichotangulia ili maana itimie.

[2] Al-Maa'uwn (107: 4 - 5)

Khitilafu hizo zipo pia katika sehemu nyinginezo za Qur-aan mfano kusimama katika neno la: الزَّقُّوم katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) Suwratud-Dukhaan (44: 43, 44)

إِنَّ شَجَرَتَ ٱلزَّقُّومِ ٤٣ طَعَامُ ٱلۡأَثِيمِ ٤٤

kwenye Aayah namba 4 kisha likatokea jambo la kumshughulisha msomaji akafunga msahafu kukusudia kumaliza kisomo chake bila ya kuunganisha na yanayofuatia.

Sababu ya hayo ni kwamba Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema katika Aayah hiyo ya mwanzo: **((Basi, ole kwa wanaoswali))**. Vipi basi wanaoswali iwe ole kwao (yaani waangamie motoni)? Ndipo inapobidi kuendelea kuleta maana iliyokusudiwa kwamba: **((Ambao wanapuuza Swalah zao))[4].**

Mfano wa nne mwishoni mwa Aayah:

Kusimama mwisho wa Aayah ya kwanza juu ya kuwa inafungamana kimaana na kilugha na Aayah ya pili yake.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمُزَّمِّلُ ۝١ قُمِ ٱلَّيۡلَ إِلَّا قَلِيلٗا ۝٢

((Ee uliyejifunika!)) ((Simama [kuswali] usiku kucha isipokuwa [muda] mdogo tu))[5]

Aayah ya pili imeanza na 'kitenzi cha kuamuru' (فِعْلُ أَمْرٍ) **"Simama usiku"** ambacho bila shaka kinahitaji maelezo ya anayepewa amri hiyo. Kwa hiyo haipendezi kuanzia Aayah ya pili bila ya Aayah ya kwanza.

Mfano wa tano mwishoni mwa Aayah:

﴿ ۞ يَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلۡخَمۡرِ وَٱلۡمَيۡسِرِۖ قُلۡ فِيهِمَآ إِثۡمٞ كَبِيرٞ وَمَنَٰفِعُ لِلنَّاسِ وَإِثۡمُهُمَآ أَكۡبَرُ مِن نَّفۡعِهِمَاۗ وَيَسۡـَٔلُونَكَ مَاذَا يُنفِقُونَ قُلِ ٱلۡعَفۡوَۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمُ ٱلۡأٓيَٰتِ لَعَلَّكُمۡ تَتَفَكَّرُونَ ۝٢١٩ فِي ٱلدُّنۡيَا وَٱلۡأٓخِرَةِۗ ...

((Wanakuuliza kuhusu ulevi na kamari. Sema: "Humo [katika viwili vyote] mna dhambi kubwa na [pia mna] manufaa kwa watu. Na dhambi yake [vitu viwili hivyo] ni kubwa kuliko manufaa yake." Na wanakuuliza nini watoe. Sema: *"Al-'Afwa*

[4]Al-Maa'uwn (107: 5)
[5] Al-Muzzammil (73: 1-2)

[yaliyokuzidieni].” Hivyo ndivyo Allaah Anavyokubainishieni Aayaat mpate kutafakari)) ((Katika dunia na Aakhirah ...))[6]

Bonyeza usikilize

Kusimama mwisho wa Aayah ya kwanza juu ya kuwa inafungamana kimaana na kilugha na yanayoanzia Aayah ya pili yake; فِي الدُّنْيا وَالآخِرة ambayo ni جَرٌّ وَ مَجْرُورٌ *jarrun wa majruwr* (kihusishi na kinachohusishwa). Hapa kuna uhusiano wa kilugha na pia inahusiana na maana (فِعْلٌ) *fi'lun* (kitendo) cha 'kutafakari' تَتَفَكَّرُونَ katika Aayah iliyoishia[7]. Kwa vile imetokea mwisho wa Aayah inaruhusiwa kusimama na kuanza Aayah ya pili inayofuata kwa sababu ndivyo ilivyothibiti katika Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kusimama katika kila Aayah. Lakini ingelikuwa katikati ya Aayah basi isingelipasa kuanzia katika maneno kama hayo.

- Mfano wa kwanza katikati ya Aayah:

  Kusimama katika neno:

  ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ

  ((*Alhamduli-Llaah* [Sifa njema zote ni za Allaah]))

  Katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

  ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ۝٢

[6] Al-Baqarah (2: 219-220)

[7] Wanavyuoni wamefafanua kuhusu uhusiano wa kutafakari duniani na Aakhera kuwa amri za Allaah (سبحانه وتعالى) zinahuisana na maslahi ya kidunia na Aakhirah. Aayah mbili hizo zimetaja maovu ya kujiepusha nayo; ulevi , kamari na zimetaja pia mema ya kutekeleza kama kutoa mali kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) na kuwalea mayatima. Na Allaah (سبحانه وتعالى) Anajua zaidi

((*Alhamduli-Llaah* [Sifa njema zote ni za Allaah] Mola wa walimwengu))[8].

Kusimama kama hapa maneno yanaeleweka na yanaleta maana sahihi kabisa na ni maana yenye kukubalika na ni kisimamo kizuri: **((*Alhamduli-Llaah* [Sifa njema zote ni za Allaah])),** lakini inafungamana na yanayofuatia kilugha na kimaana; hivyo japokuwa kusimama kunapendeza lakini hakupendezi kuanza na yanayofuatia; kwa hivyo inapendekezwa na ni vizuri yarudiwe kusomwa ili aendelee kuunga na yanaofuatia nayo ni:

رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ

((...Mola wa walimwengu))

- Mfano wa pili katikati ya Aayah:

  Kusimama katika neno:

  فَسَجَدُوٓاْ

  ((wakasujudu))

  Katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

وَإِذۡ قُلۡنَا لِلۡمَلَٰٓئِكَةِ ٱسۡجُدُواْ لِأٓدَمَ فَسَجَدُوٓاْ إِلَّآ إِبۡلِيسَ أَبَىٰ وَٱسۡتَكۡبَرَ وَكَانَ مِنَ ٱلۡكَٰفِرِينَ ﴿٣٤﴾

((Na [taja] Tulipowaambia Malaika: "Msujudieni Aadam." Wakasujudu isipokuwa Ibliys alikataa na akatakabari na akawa miongoni mwa makafiri))[9]

Kusimama hapo kauli inaeleweka na inaleta maana sahihi. Lakini haifai kuanzia yanayofuatia kwa sababu yanafungamana kimaana na kilugha; hivyo bila ya kuendelea haitaleta maana ilokusudiwa kwamba Malaika wote walisujudi **ispokuwa Ibliys**. Kwa hiyo lazima kurudia maneno ya nyuma kidogo ili kuunganisha na yanayofuatia.

---

[8] Al-Faatihah (1: 2)
[9] Al-Baqarah (2: 34)